

# MKATABA WA UPANGISHAJI

Mkataba huu unafanywa leo tarehe 1 Mwezi wa 10 mwaka 2021

## KATI YA

**AMNEY ABDULKARIM** wa S.L.P 106 DAR ES SALAAM  
ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MPANGISHAJI**

## NA

**CYTECH INKS TANZANIA LIMITED** WA S.L.P 11303 DAR ES SALAAM mbye katika mkataba huu  
atajulikana kama **MPANGAJI**.

Na kwa vile **MPANGISHAJI** ana nia na yuko tayari kupangisha office yake iliyopo katika mtaa wa  
Lumumba na bibititi road city mall building Wilaya ya ilala Mkoa wa Dar es salaam

### **KWA HIYO MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

1. Kodi itakayolipwa na mpangaji kwa mpangishaji katika mkataba huu wa upangaji ni shilingi za  
kitanzania **TSH 300,000** kwa mwezi ambazo zitalipwa kwa kipindi cha miezi mitatu  
kuanzia tarehe ya kusaini mkataba huu. Office inaukubwa wa sq mita 12
2. Wajibu na majukumu ya mpangaji katika mkataba huu ni kama ifuatavyo:
  - (a) Kulipa kodi yote iliyotajwa katika mkataba huu kadri ya makubaliano.
  - (b) Wakati wote wa ukaazi katika offic, kutunza na kuweka mazingira yote ya office (ndani  
na nje) katika hali ya usafi wote na kuhakikisha utunzaji wa vifaa vyote vya office  
ikiwamo milango, vitasa, madirisha, nyaya za umeme, rangi na mazingira kwa ujumla  
yawe katika hali nzuri wakati wote.
  - (c) Kumruhusu mpangishaji au wakala wake atakaye mteua kuingia katika office kwa ajili  
ya ukaguzi na au kufanya matengenezo.  
Kuingia huko katika office lazima kuwe kwa wakati na muda unaokubalika hasa wakati  
wa mchana na lazima kuwe na taarifa kutoka kwa mpangishaji itakayokuwa imetolewa  
kwa mpangaji kwa muda muafaka.
  - (d) Kutokubadilisha mandhari ya office, kuongeza au kupunguza  
Chochote kisichohamishik pasipo kuomba na kupatiwa idhini ya kimaandishi na  
mpangishaji.
  - (e) Kutumia office inayohusika na mkataba huu kwa kazi za office tu na kutoruhusu au  
kuweka kitu chochote ambacho kitasababisha kero, usumbufu, au kuwa chanzo cha  
uharibifu wa office na / au mazingira ya office au office za jirani.
  - (f) Kutokufanya biashara ya aina yeyote katika office, na kutokuifadhi vitu vya kulipuka km  
petrol, diesel na gesi.
  - (g) Kulipa na kua zote zitokanazo na matumizi ya umeme na maji na kuhakikisha wakati  
wote haachi deni lolote litokanalo na matumizi tajwa katika kipindi chote cha ukaazi.



- (h) Kutokupangisha office inayohusiana na mkataba huu au sehemu yeyote ya office kwa mpangaji mwengine. Mpangaji atakapoondoka anatakiwa kukabidhi office kwa mpangishaji au mwakilishi wake atakayemwarifu.
- (i) Mkataba huu utakapokoma au kwisha kipindi chake na ikiridhiwa na pande zote mbili kutokuendeleza mpangaji atatakiwa kukabidhi office kwa mpangishaji ikiwa katika hali nzuri pamoja na vifaa vyote vya office ikiwemo milango, vitasa, madirisha, mabomba, nyaya za umeme. Kama alivyokabidhiwa mwanzoni mwa mkataba. Mpangaji atatakiwa kulipa na/kufidia uharibifu wowote utakaotokana na matumizi mabaya na yasiyo ya kawaida au sahihi katika office

3. Wajibu na majukumu ya Mpangishaji katika Mkataba huu ni kama ifuatavyo:

- (a) Kukabidhi office na maeneo yanyoambatana nayop yanayohusiana na mkataba huu wa upangaji mara baada ya pande zote kutia sahihi katika mkataba huu.
- (b) Kutunza na kuweka office ya upangaji katika hali ya kukalika wakati wot na kufanya matengenezo ya uchakavu wa kawaida mara taarifa inapotolewa na mpangaji.
- (c) Kuhakikisha kwamba mpangaji anakaa kwa amani na anafurahia office na eneo linaloambatana nalo bila kubughudhiwa kwa namana yeyote na mpangishaji au mwakilishi wake kwa kipindi chote cha mkataba huu.

4. Kwa sharti kwamba inakubalika na kutamkwa na pande zote mbili kuwa :

- (a) Kama kutakuwa hakuna ukiukwaji wowote wa mkataba huu na Mpangaji ametoa taarifa kwa Mpangishaji miezi (2) kabla ya mkataba huu kufika kikomo kukusudia kuuendeleza mkataba huu, na kama mpangaji ataridhia, mkataba huu utatiwa saina tena kwa kipindi kipya na pande zote mbili kwa masharti yale yale au tofauti na yale yaliyokuwa kwenye mkataba huu.
- (b) Ikitokea Mpangaji amekatisha mkataba kabla ya kipindi kilichokubaliwa kwenye mkataba kwisha, mpangishaji atamrudishia nusu ya fedha itakayokuwa imebaki kwenye mkataba.



Kwa kuridhia na kuthibitisha dhamira zetu, pande zote mbili zinasafikiwa na penzile vyote vya mkataba huu na kuweka saina.

Jina Mpangishaji

Saini

AMNEY ABDULKARIM

*[Signature]* 01/10/2021

Jina Mpangaji

Saini

C/o Rabiach Mtage Alkavithy  
CYTECH INKS TANZANIA LIMITED

*[Signature]* 01 OCTOBER 2021

Tarehe... 1... Mwezi... 10... mwaka... 2021

153-703-841

Sl duty 36000

WH 90000 (3 months) 1 Oct - 31 Dec 2021

126000

11/10/2021

Winnie



MUSA A. ROMA  
ADVOCATE STAMP DUTY

*[Signature]* 36000 Collected  
998414512394 13/10/2021  
Receipt No: Date:

Regional Manager - Ilala Tax Region